TANGAZO LA SERIKALI NA. 551 la TAREHE 26 Jul 2019

# SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)
*(Imetolewa chini ya kifungu cha 28(1)(d))*

## AMRI YA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KILOLO ("KILOLO WSSA")

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Marekebisho ya Bei ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kilolo ("Kilolo WSSA"), ya mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa kuanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Kilolo WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 30 Septemba 2019 au kabla, Kilolo WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Kilolo WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(c) Kilolo WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(d) Kilolo WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa

masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

Sura 414
G.N.No.193 of 2010

(e) Kilolo WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Kilolo WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Kilolo WSSA katika siku zijazo; na

(f) kuanzia tarehe 1 Agosti 2019, Kilolo WSSA itaanza kulipa tozo ya EWURA kwa mujibu wa kifungu namba 43 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na kifungu cha 6 cha Kanuni za EWURA kuhusu Taratibu za Kukusanya ada na tozo zilizochapishwa katika Tangazo la Serikali Namba 193 la mwaka 2010.

Amri Na. 11-014

**5**. Amri hii inasitisha matumizi ya Amri Na. 11-014 ya tarehe 1 Juni 2011 katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kilolo (Kilolo WSSA).

*Tangazo La Serikali Na. 551 (linaendelea)*

JEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali la 1(a): Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa kwa wateja wenye dira (Shilingi/ mita ya ujazo)

| Kundi la wateja | Matumizi (mita za ujazo) | Bei za sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 0-5 | 445 | 1,300 | 1,480 | 1,590 |
| | 5> | 465 | 1,360 | 1,550 | 1,660 |
| Taasisi | | 470 | 1,370 | 1,560 | 1,680 |
| Biashara | | 600 | 1,650 | 1,710 | 1,790 |
| Magati | | 1,250 | 1,250 | 1,250 | 1,250 |
| Viwandani | | 600 | 1,650 | 1,710 | 1,790 |
| Wastani | | 549 | 1,450 | 1,640 | 1,760 |

Jedwali la 1(b): Bei ya sasa na iliyoidhinishwa kwa wateja wasio na dira (Shilingi kwa mwezi)

| Kundi la wateja | Matumizi (mita za ujazo) | Bei za sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 1 – 5 | 4,500 | Bei ya maji kwa wateja wasio na dira zimeondolewa | | |
| | | 5,500 | | | |
| Biashara | 1 – 5 | 9,400 | | | |
| | 6--10 | 17,000 | | | |
| Taasisi | 1 – 5 | 12,000 | | | |
| | 5> | 22,000 | | | |
| Viwandani | 1 – 5 | 13,000 | | | |
| | 6--10 | 22,500 | | | |

Jedwali Namba 1(c): ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya maunganisho ya maji safi (Shilingi/maunganisho)

| Kundi la wateja | Current fees | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 32,000 | Asilimia 20 ya gharama za maungansho kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 24 cha kanuni za maji za mwaka 2013. | | |
| Biashara | 51,500 | | | |
| Taasisi | 51,500 | | | |
| Viwandani | 53,500 | | | |

*Tangazo La Serikali Na. 551 (linaendelea)*

Jedwali la 1(d): Ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya kurejeshewa huduma ya maji baada ya kukatiwa (Shilingi/kurejeshewa huduma)

| Kundi la wateja | Ada ya sasa | Ada ziliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 26,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 26,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 26,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

## JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Na | Maelezo | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|
| | | Shilingi | Shilingi | Shilingi |
| UkarabatinaKubadilisha | | | | |
| 1 | Ukarabati wa mtego (Intake) wa maji Na. I, II, III na IV kwa kubadili mabomba ya umbal iwa mita 200m aina PVC yenye kipenyo cha150mm ya kuchujamaji (machujio) (infilitation gulliries) pamoja na kujenga fensi. MtegoNamba II na II kwamwaka 2019/20 naMtego Na. III kwamwakawafedha 2020/21 naMtego Na. IV kwawafedha 2021/22 | 5,000,000 | 5,000,000 | 5,000,000 |
| 2 | Kubadilisha mabomba chakavu umbal i wa kilometa 0.9 za plastiki (PVC and HDPE ) zenye kipenyo cha 110mm, 63mm na 90mm kwenye bomba kuu la maji safi kutoka chanzo cha maji Mwosongela kwenda kijiji cha Utengule kwa wastani wa kilometa 0.3 kwa kila mwaka. | 8,855,148 | 8,855,148 | 8,855,148 |
| 3 | Ukarabati wa Matenki matatu (3) ya maji maeneo ya Lusinga, Utengule pamojanakujengafensi. tenkimoja la Lusinga kwa mwaka wa fedha 2019/20 na | 6,000,000 | 6,000,000 | 0 |

*Tangazo La Serikali Na. 551 (linaendelea)*

| Na | Maelezo | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|
| | Matenki mawili ya Utengule kwa mwaka wa fedha 2020/21. | | | |
| | Jumla ndogo - ukarabati | 19,855,148 | 19,855,148 | 13,855,148 |
| Uwekezaji mpya | | | | |
| 4 | Kuchimba kisima kirefu kimoja eneo la kibaoni pamoja na kujenga mtandao wa kupeleka maji kwenye tank km 1, kuweka umeme, kufunga pampu kujenga kibanda cha pampu | | | 43,000,000 |
| 5 | Kuongeza mtandao wa majisafi km 4 kwa kutumia mabomba yenye kipenyo cha 63mm - 32mm kwenye kijiji cha Luganga, Luhindo and Lulanzi. kilometa 2 kwa mwaka wa fedha 2019/20 na kilometa mbili nyingine kwa mwaka wafedha 2020/21. | 37,000,000 | 37,000,000 | |
| | Jumla ndogo - gharama za uwekezaji mpya | 37,000,000 | 37,000,000 | 43,000,000 |
| | Jumla kuu ya gharama za kukarabati, kubadilisha, na uwekezaji mpya | 56,855,148 | 56,855,148 | 56,855,148 |

## JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

| Maelezo | Kipimo | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 70 | 70 | 70 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 29 | 28 | 27 |
| Wateja wenye dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 95 |

*Tangazo La Serikali Na. 551 (linaendelea)*

## JEDWALI LA NNE

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA(Milioni TZS)

| GHARAMA | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| | Zilizoidhinishwa | Zilizoidhinishwa | Zilizoidhinishwa |
| Uzalishajiwa maji | 8.13 | 13.60 | 14.49 |
| Usambazajiwa maji | 7.36 | 7.42 | 11.64 |
| Matengenezo | 5.40 | 8.07 | 8.40 |
| Watumishi | 30.74 | 40.60 | 40.66 |
| Utawala | 16.95 | 26.98 | 48.65 |
| Matangazo | 1.30 | 1.80 | 2.00 |
| Matukio | 0.60 | 3.00 | 3.00 |
| Gharama za benki | 0.07 | 0.07 | 0.07 |
| Bodi | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Jumla (Uendeshajina matengenezo) | 70.55 | 101.54 | 128.91 |
| Uchakavu | 56.86 | 56.86 | 56.86 |
| Jumla ya gharama zote | 127.41 | 158.40 | 185.77 |
| Toa: Mapatomengineyo | 5.84 | 5.85 | 6.16 |
| Mapato yatokanayo na mauzo ya maji | 121.57 | 152.54 | 179.60 |

Dodoma
....., 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*